Chuo Kikuu cha Dar es Salaam

HEKIMA NI UHURU

HEET
HIGHER EDUCATION FOR ECONOMIC TRANSFORMATION

Toleo la 03

# Jarida la HEET UDSM

**Toleo la Oktoba 2023**

**HEET**

**Elimu ya Juu kwa Mageuzi ya Kiuchumi**



**Serikali yaitangaza rasmi Kampasi Mpya ya UDSM Lindi**

uk 6




**Chuo Kikuu cha Dar es Salaam Kujenga Majengo 24 Kupitia Mradi wa HEET**

uk 8



UDSM yapokea Magari na Vifaa vya TEHAMA Kuboresha Ufundishaji na Ujifunzanji kwa Wanafunzi wenye Mahitaji Maalum

uk 18

# Yaliyomo


*Salamu za Makamu Mkuu wa Chuo* 3

*Ujumbe wa Mratibu wa HEET* 4

*Serikali yaitangaza rasmi Kampasi Mpya ya UDSM Lindi* 6

*Programu 200 Zatathminiwa katika Mchakato wa Mapitio ya Mitaala UDSM* 7

*Chuo Kikuu cha Dar es Salaam Kujenga Majengo 24 Kupitia Mradi wa HEET* 8

*Wanufaika wa kundi la kwanza wanaofadhiliwa na Mradi wa HEET Wahitimu* 10

*Kutoka Mezani kwa Naibu Mratibu wa HEET UDSM* 11

*Kikao cha Kamati ya Usimamizi wa Mradi, Oktoba 2023* 12

*Tahariri* 13

*Matukio katika Picha* 14

*Maafisa Rasilimaliwatu UDSM wajengewa uwezo wa namna ya kushughulikia malalamiko* 16

*Maafisa Mawasiliano Wakubaliana Mkakati wa Kutangaza Mradi wa HEET* 17

*UDSM Yapokea Magari na Vifaa vya TEHAMA Kuboresha Ufundishaji na Ujifunzanji kwa Wanafunzi wenye Mahitaji Maalum* 18

*UDSM yaanzisha Ofisi ya Ushirikiano baina ya Chuo na Waajiri* 19

*Waratibu Wapewa Mafunzo kuhusu Usimamizi wa Vituo vya Uatamizi na Ubunifu* 20

*UDSM, TPSF na Watendaji Wakuu Wafanya Mdahalo Kuhusu Wahitimu na Soko la Ajira* 21

*Miundombinu ya Mtandao UDSM Kuboreshwa ili Kuimarisha Mawasiliano ya Dijitali* 22

*Sera na Miongozo Mbalimbali Vyaandaliwa UDSM* 23

# Salamu za Makamu Mkuu wa Chuo



Prof. William A. L. Anangisye

**Makamu Mkuu wa Chuo**

Ninatumia fursa hii kuwakaribisha wasomaji na marafiki zetu wote katika toleo la Jarida hili la HEET-UDSM. Kwa kuzingatia kwamba Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kimekwishatimiza mwaka mmoja tangu kilipoanza utekelezaji wa Mradi wa HEET ni dhahiri kwamba kuna hatua kadhaa zimepigwa. Mwaka wa kwanza kiasi kikubwa umejikita zaidi katika kuweka sawa mpangilio na kupeana maelekezo.

Kwa kiasi kikubwa mwaka huu umejikita katika kuweka sawa muundo wa mradi, mpangilio wa utekelezaji na kuwaandaa wadau kwa ajili ya majukumu yatakayofanyika mwaka wa pili. Kama tulivyofanya mwaka uliopita, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kimedhamiria kuhakikisha kwamba utekelezaji wa shughuli mbalimbali za Mradi wa HEET unakwenda vyema na kwa ufanisi.

Utelezaji wa Mradi wa HEET unakwenda sambamba na Dira ya Maendeleo Tanzania 2025, Awamu ya Tatu ya Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano 2021/22-2025/25 na Ilani ya Chama cha Mapinduzi (2020-2025). Vipaumbele hivi vya Taifa vinalenga kuleta mabadiliko ya kiuchumi kwa kuzingatia zaidi kujenga uchumi wa viwanda, kukabiliana na hali ya nchi ya kipato cha kati na kukuza fursa za ajira kwa makundi mbalimbali hususani vijana ambao ni sehemu kubwa ya nguvukazi ya taifa.

Katika ngazi ya Chuo, kumeandaliwa Mpango Mkakati wa Uwezekazaji wa Chuo kwa ajili ya Mradi wa HEET unaoenda sambamba na Dira ya Chuo ya mwaka 2061 na Mpangomkakati wa Chuo (ulioboreshwa) kwa mwaka 2020/21-2024/25. Matokeo yanayotarajiwa katika Mradi wa HEET ni kuwa na mageuzi katika mitaala ya Chuo na miundombinu inayohusiana na mitaala hiyo ili kuhakikisha kwamba shughuli za ufundishaji, utafiti na huduma kwa jamii zinaendana na mahitaji halisi ya jamii.

Mageuzi ya kimkakati katika Mradi wa HEET yanalenga kukuza uhusiano kisekta (umma na binafsi) kwa kuzishirikisha sekta hizo katika majukumu ya msingi ya Chuo. Kupitia Mradi huu wanataaluma wamepata ufadhili kusoma Programu za Uzamili nje ya nchi. Viongozi wa Chuo pia wamepata fursa ya kuhudhuria mafunzo ya muda mfupi. Muhimu zaidi ni kwamba mara mradi huu utakapokamilika mfumo wa TEHAMA utakuwa umeingizwa kikamilifu katika shughuli zote za msingi zinazoendeshwa ndani ya Chuo. Hali hii itatuhakikishia ufanisi katika matumizi ya rasilimali na utendaji wa kila siku na hivyo kuleta mapinduzi chanya katika kuwahudumia wateja.

Chuo kimepanga kujimarisha katika tafiti na ubunifu na hivyo kuendelea kulinda hadhi yake ya kuwa kinara katika shughuli za utafiti na ufundishaji katika elimu ya juu nchini Tanzania. Hivyo basi, ili kufikia malengo hayo, Chuo kimedhamiria kuhakikisha kwamba kuna ushirikishwaji wa kutosha katika shughuli zote za kimkakati. Katika kipindi chote cha utekelezaji wa mradi na katika shughuli zote zinazofanyika, Chuo kimechukua hatua zote zinazohitajika kupunguza athari za kimazingira na kijamii.

Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kinaishukuru Benki ya Dunia kwa kuiwezesha Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia katika utekelezaji wa Mradi wa HEET. Chuo kinaahidi kutekeleza kwa ukamilifu shughuli zote za Mradi kama zilivyoainishwa katika Mkataba na Mpangomkakati wa Uwekezaji na hivyo kufanikisha kwa ufanisi utekelezaji wa Lengo la Maendeleo ya Mradi.

Mwaka wa pili wa utekelezaji wa Mradi utakuwa muhimu sana kwa Chuo kwa kuwa ndicho kipindi ambacho ujenzi wa majengo na usimikaji wa miundombinu ya mfumo wa kidijitali utaanza. Hivyo, Menejimenti ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam iko makini kuhakikisha kwamba shughuli hizi za mradi zinatekelezwa kwa kuzingatia msingi wa uwazi, ushindani, uadilifu na thamani halisi ya fedha.

Kwa mara nyingine ninawakaribisha wasomaji wetu kusoma kwa furaha Jarida la HEET-UDSM. Tunafurahia na kuthamini sana ushirikiano wenu. Tafadhali msisite kutuma maoni yenu kuhusu Jarida na utekelezaji wa Mradi wa HEET kwa ujumla.

# Ujumbe wa Mratibu wa HEET



## Prof. Bernadeta Killian

## Mratibu wa Mradi wa HEET-UDSM

Ninafurahi kuripoti kwamba utekelezaji wa majukumu ya Mradi wa HEET unaendelea vyema Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Tulikuwa na mwaka mmoja wenye mafanikio makubwa katika hatua ya awali ya utekelezaji wa Mradi. Kwa kuzingatia kwamba huu ni mwaka wa kwanza kati ya miaka mitano ya muda wa Mradi, tumeunda timu imara na kujifunza kufanya kazi pamoja.

Tumejenga utamaduni wa ushirikiano katika utendaji kazi na kufikia matarajio ya wadau. Muhimu zaidi ni kwamba tumekubaliana kusonga mbele tukiwa na matarajio ya hali ya juu ya kufanikisha utekelezaji wa majukumu tuliyojipangia.

Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kimepokea Dola za Kimarekani milioni 47.5 kwa ajili ya utekelezaji wa Mradi wa HEET kwa kipindi cha miaka 5 kuanzia Julai 2021 hadi Julai 2026. Lengo kuu la Maendeleo ya Mradi ni kuboresha mazingira ya ujifunzaji na kujenga uhusiano baina ya mahitaji ya soko la ajira na programu za kipaumbele katika Taasisi za Elimu ya Juu na kuboresha usimamizi wa mfumo wa elimu ya juu nchini. Kwa upande wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam tumeteua programu tano za kipaumbele. Programu hizo ni: Uhandishi na Teknolojia, Kilimo na Kilimobiashara; Teknolojia ya Habari na Mawasiliano; Uhandisi Mazingira na Teknolojia na Masuala ya Utalii na Ukarimu

Lengo kuu la Maendeleo ya Mradi linatekelezwa kwa kuzingatia maeneo nane ya kipaumbele ambayo ni:

- Ujenzi na ukarabati wa miundombinu
- Kufanya mapitio ya mitaala na kuzingatia methodolojia ya ubunifu katika ufundishaji
- kukuza utafiti na ubunifu;
- kujenga ushirikiano wa kisekta (za umma na binafsi);
- kuimarisha matumizi ya teknolojia ya dijitali katika ufundishaji;
- Kukuza uwezo wa ndani wa kuzalisha mapato;
- Kuwajengea uwezo wanataaluma na viongozi wa Chuo na;
- Usimamizi, Uratibu, Ufuatiliaji na Tathmini ya Mradi.

Utekelezaji wa Mradi huu ulianza tarehe 19 Juni 2022 baada ya kusainiwa kwa mkataba na kupokea awamu ya kwanza ya fedha mwezi Agosti 2022. Zaidi ya asilimia 75 fedha za Mradi wa HEET imeelekezwa katika kuboresha miundombinu na kuimarisha rasilimali za kujifunzia.

Katika mwaka wa kwanza wa utekelezaji wa Mradi, shughuli kadhaa za Mradi zimetekelezwa na nyingine maendeleo yake yanaridhisha kama ifuatavyo:

Mosi, kwa upande wa ukarabati na ujenzi wa miundombinu, Chuo kimekwishafanya uchunguzi wa kijiografia, kitopografia na kuandaa michoro. Pili, Chuo kimesaini mkataba na washauri elekezi wawili kwa ajili ya kusanifu, kufanya mapitio na kusimamia ujenzi wa majengo 24 yatakayojengwa Dar es Salaam, Zanzibar na Lindi. Wakandarasi wanapaswa kuwa kwenye maeneo ya ujenzi mwishoni mwa mwezi Disemba, 2023 baada ya kukamilika kwa michakato inayohitajika. Ujenzi utazingatia athari za kimazingira na kijamii.

Tatu, Chuo kimekamilisha utafiti fuatilizi. Zoezi hili lilihusisha wahitimu 8,000 na waajiri 3,000 pamoja na wadau wengine kama vile Kamati mbalimbali za Ushauri katika sekta ya ajira. Matokeo yaliyopatikana kupitia utafiti fuatilizi yatakuwa na msaada mkubwa wakati wa mapitio ya mitaala kazi inayoendelea hivi sasa katika vitengo mbalimbali vya kitaaluma. Nne, Chuo kimetoa ufadhili kwa wanataaluma 23 kusoma masomo ya uzamili (10 Umahiri na 13 Uzamivu). Tunafurahi kuripoti kwamba wanufaika wanne wa ufadhili huu wamehitimu digrii zao za umahiri na wamekwisharejea kazini.

Tano, kuhusiana na kujenga ushirikiano na sekta mbalimbali, shughuli kadhaa zimefanyika kuanzia Julai 2022. Miongozo mbalimbali kufanikisha ushirikiano huu imeandaliwa. Miongoni mwa maeneo yaliyoangaziwa na utekelezaji wake unaendelea ni fursa maalum za kazi kwa wanyakazi na mazoezi kwa vitendo kwa wanafunzi, programu maalumu ya mikataba ya ajira kwa wafanyakazi na ushirikiano katika shughuli za utafiti na ubunifu.

Ili kufanikisha ushirikiano uliokusudiwa, makundi matano ya Kamati za Ushauri yemeundwa katika nyanja za Sayansi ya Bahari; TEHAMA na Vyombo vya Habari; Uhandisi na Rasilimaliardhi; Uchumi, Kilimo na Biashara;  Insia, Sayansi za Jamii na Rasilimali. Kila Kamati ilibainisha walau maeneo mawili ya ushirikiano. Ofisi mpya ya Ushirikiano iliyoanzishwa chini ya Kurugenzi ya Huduma kwa Umma itaendelea kujenga na kuimarisha ushirikiano baina ya Chuo na sekta mbalimbali hususan sekta binafsi. Utaratibu wa ushirikiano umerasimishwa kwa kusainiwa mikataba mitatu ya maridhiano kwa kuanzia. Matunda ya kusainiwa kwa mikataba hii ni kupatikana kwa fursa ya mkataba maalum kiwandani kwa wanataaluma wawili.

Aidha, kwa lengo la kuongeza idadi ya wanawake katika Sayansi, Teknolojia, Uhandisi na Hisabati, Timu ya kutoka Kurugenzi ya Jinsia na Kituo cha huduma kwa watu wenye mahitaji maalum ilifanya warsha ya uhamasishaji kwa wanafunzi wa kike 3,083 wa shule za sekondari kutoka maeneo ya Zanzibar, Morogoro, Kagera, Lindi, Mtwara na Mbeya. Mwisho ingawa siyo kwa umuhimu wafanyakazi kutoka vitengo vya rasilimaliwatu, utawala, ulinzi na miliki walipatiwa mafunzo kuhusu mikakati ya kushughulikia malalamiko.

Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kinathamini ushirikiano kilioupata kutoka kwa wadau wa ndani na nje katika kufikia mafanikio muhimu kiliyoyapata katika kipindi hiki huku tukiamini kwamba ushirikiano huu utaendelezwa katika hatua zinazofuata za utekelezaji wa Mradi wa HEET.



***Mratibu wa Mradi wa HEET Chuo Kikuu cha Dar es Salaam Prof. Bernadeta Killian akiongea katika moja ya mikutano ya watendaji wa mradi huu chuoni***



*Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda (Mb) (wa pili kushoto) akitazama ramani inayoonesha eneo ambapo Kampasi mpya ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam Mkoani Lindi inajengwa. Wengine wanaotazama ni Mratibu wa Mradi wa HEET-UDSM na Naibu Makamu Mkuu wa Chuo-Mipango, Fedha na Utawala, Prof. Bernadeta Killian (wa tano kushoto) na wataalamu kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na Maafisa kutoka Ofisi ya Mkoa, Lindi. Hii ilikuwa katika eneo hilo la Kampasi ya UDSM, Mkoani Lindi, tarehe 22 Mwezi Agosti, 2023.*

# Serikali yaitangaza rasmi Kampasi Mpya ya UDSM Lindi

***Na Dotto Kuhenga, UDSM-HEET***

Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia Mhe. Prof. Adolf Mkenda ametangaza rasmi kuanzishwa kwa Kampansi mpya ya Lindi ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Akizungumza mjini Lindi Agosti 22, 2022, Mhe. Waziri alisema kwamba hatua zote za kujenga kampasi mpya ikiwa ni pamoja kutolewa kwa tangazo Na. 569 katika Gazeti la Serikali zimezingatiwa hivyo ujenzi wa miundombinu unaweza kuanza mwezi Novemba 2023.

Akitoa tamko rasmi la kutambua Kampasi hii Prof. Mkenda amesema: "Ninatangaza rasmi kwamba sasa maeneo yaliyoteuliwa ya Ngongo na Ruangwa ni Kampasi ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Kampasi mpya ya Lindi na kwamba ujenzi wa wa majengo yakiwemo madarasa utaanza rasmi Novemba 2023".

Kwa upande wake Naibu Makamu Mkuu wa Chuo, Mipango, Fedha na Utawala ambaye pia Mratibu wa Mradi wa HEET UDSM Prof. Bernadeta Killian amesema kampasi mpya ya Lindi itakuwa ni mahususi kwa fani za Kilimo, ufugajinyuki, teknolojia ya chakula na programu nyingine zinazohusiana na hizo. Aidha, alitumia wasaa huo kuishukuru Benki ya Dunia kupitia Mradi wa HEET kwa kutoa fedha za kutekeleza Mradi huu.

Januari, 2023 Mkuu wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na Rais Mstaafu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Jakaya Kikwete alieleza namna ambavyo Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kimejipanga kufungua kampasi mpya katika Wilaya ya Ruangwa na Manispaa ya Lindi kwa lengo la kupanua wigo na kuongeza fursa ya mafunzo ya elimu ya juu kwa Watanzania wote.

Mhe. Kikwete aliyasema hayo wakati akizungumza na viongozi na wananchi alipotembelea maeneo ya Ngongo na Kitandi katika manispaa ya Lindi na Wilaya ya Ruangwa mtawalia.

"Tunapenda kuwahakikishia kwamba tuna dhamira ya dhati ya kuanzisha kampasi mpya hapa Lindi. Ni wajibu wenu sasa kufanya kazi kwa karibu na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam katika maandalizi yanayohitajika ili mradi uendeshwe kwa wakati", alisema Mhe. Kikwete.

Amesisitiza kwamba Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kimejiandaa kuanza ujenzi wa majengo mbalimbali katika Kampasi zake kwa kuwa kimepata fedha kutoka serikalini kupitia Mradi wa Elimu ya Juu kwa Mageuzi ya Kiuchumi (HEET).

Katika ziara yake Mhe. Kikwete aliongozana na Mhe. Salma Kikwete Mbunge wa Jimbo la Mchinga; Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Prof. William Anangisye na viongozi wengine wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam pamoja na viongozi wa Manispaa ya Lindi Wilaya ya Ruangwa.

Kwa upande wake Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam Prof. William Anangisye amesema kwamba Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kimejiandaa kufanikisha shughuli za ujenzi wa kampasi hiyo mpya kwa wakati ili ianze kufundisha programu za kitaaluma zinazoendana na mahitaji ya jamii na wakati.

# Programu 200 Zatathminiwa katika Mchakato wa Mapitio ya Mitaala UDSM

Na Jackson Isdory, UDSM-HEET



Majadiliano kuhusu mapitio ya mitaalala katika Shule Kuu ya Sheria Chuo Kikuu cha Dar es Salaam



Majadiliano kuhusu mapitio ya mitaala katika Taasisi ya Tathmini ya Rasilimali Chuo Kikuu cha Dar es Salaam

Katika kuelekea hatua ya mafanikio ya elimu ya juu nchini Tanzania, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kimefanikisha mapitio ya programu zake kwa asilimia 80 ambapo zaidi ya programu 200 zimetathminiwa mapitio na mchakato kamili unatarajiwa kukamilika mapema mwakani 2024.

Akitoa maelezo kuhusu hatua iliyofikiwa katika mchakato huu ulioanza mwaka 2022, Mtaalamu wa Mitaala wa Mradi wa HEET UDSM kwa upande wa mapitio ya mitaala Profesa Masoud Muruke amesema kwamba kuna matumaini makubwa kwa kuwa vitengo mbalimbali vimepiga hatua katika mchakato huu kwa kukamilisha jukumu hili kwa kati ya asilimia 70 hadi 90.



**Prof. Bonaventure Rutinwa**
Naibu Makamu Mkuu wa Chuo - Taaluma

"Kuanzia Julai 2022 hadi Septemba 2023 vitengo mbalimbali vya kitaaluma vimekuwa vikifanya utafiti fuatilizi na tathmini binafsi kuhusu programu zinazoendeshwa na vitengo hivyo. Vitengo vingi vilianza mchakato wa mapitio na kufanya mikutano mbalimbali ili kujenga welewa wa pamoja miongoni mwa wanataaluma wa vitengo husika. Mpangokazi wa kina uliandaliwa kisha kukatengwa bajeti kwa ajili ya kufanikisha jukumu hili", amesema Prof. Muruke.

Prof. Muruke ameeleza zaidi kwamba tathmini hii ambayo imekuwa na manufaa makubwa ilihusisha jumla ya programu 200 za shahada ya awali na uzamili. "Katika tathmini hii asilimia 60 ilifanyika kwa njia ya mtandao na asilimia 40 ilifanyika kwa njia ya ana kwa ana".

Alisisitiza kwamba, kuanzia Mwezi Julai 2022 Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kimepata mafanikio makubwa katika hatua ya maandalizi na mchakato wa mapitio ya programu. Mchakato huu, mbali na mambo mengine, ulihusisha maandalizi ya miongozo, zana za utafiti fuatilizi zilizofanyiwa majaribio, na mafunzo kwa wanajumuiya walioteuliwa kushiriki katika shughuli hii.

"Kati ya Novemba 2022 na Machi 2023 watafiti kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam walikusanya data za utafiti fuatilizi na kupata mwitiko mkubwa ambapo watoa taarifa 8,000 ambao ni sawa na asilimia 87.8 kati ya 9,111 waliotarajwa walishiriki katika utafiti huu. Data zilikusanywa kwa njia ya mtandao na nyingine kwa njia ya ana kwa ana hali iliyotoa matokeo thabiti na shirikishi", amesisitiza Prof. Muruke.

Prof. Muruke anasisitiza zaidi kwamba hatma ya safari hii ni uchambuzi uliofanywa katika vitengo vya kitaaluma ukiangazia mambo manne ya msingi ambayo ni umadhubuti, udhaifu, fursa na matishio. Tathmini hii binafsi inaweka msingi wa mapitio ya mitaala kwa kubainisha ubora na maeneo yanayohitaji kuboreshwa kwa kila programu.

Kwa upande wake Naibu Makamu Mkuu wa Chuo – Taaluma, Profesa Bonaventure Rutinwa anasisitiza kwamba mchakato huu umefanyika kwa kuzingatia miongozo na mipango ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaaam pamoja na malengo ya Mradi wa HEET.

"Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kimebainisha maeneo matano ya kipaumbe katika mchakato wa mapitio ya mitaala. Maeneo hayo ni uhandisi na teknolojia, kilimo na kilimobiashara, uhandisi mazingira na teknolojia, teknolojia ya habari na mawasiliano, uhandisi mazingira na teknolojia; masuala ya utalii na ukarimu", amesema Prof. Rutinwa

Prof. Rutinwa alieleza zaidi kwamba jitihada hizi ni hatua ya kuitikia wito wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania uliotokana na maono na maelekezo ya Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan ya kutaka kupitiwa kwa mfumo wa elimu nchini ili kuhakikisha kwamba elimu inayotolewa inaendana na mahitaji ya soko la ajira.

Kwa upande mwingine Prof. Rutinwa alieleza kwamba upitiaji wa programu ni miongoni mwa majukumu ya kawaida kwa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam ambapo jukumu hili hufanyika kila baada ya miaka kadhaa kwa lengo la kutathmini ubora wa programu zetu.



**Prof. Masoud Muruke**
Mtaalamu wa Mitaala katika Mradi wa HEET-UDSM

"Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kinafanya kazi hii kama moja ya majukumu yake ya msingi kama ilivyoelezwa katika dira na rajua, mpango mkakati, sera ya udhibiti ubora pamoja na miongozo ya kitaifa iliyotolewa na Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania", amesema Prof. Rutinwa.

Mradi wa HEET umefanikiwa kwa kupata fedha kutoka Benki ya Dunia kupitia Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambapo umekiwezesha Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kuboresha programu zake ili kuendana na soko la ajira na kuongeza ufanisi katika mfumo wa elimu ya juu nchini.

# Chuo Kikuu cha Dar es Salaam Kujenga Majengo 24 Kupitia Mradi wa HEET

*Na Dotto Kuhenga, UDSM-HEET*

Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kimesaini mikataba na kampuni mbili za ushauri elekezi kwa ajili ya kusanifu, kufanya mapitio na kusimamia mradi wa ujenzi wa majengo 21 kati 24 yaliyopangwa kujengwa chini ya Mradi wa Elimu ya Juu kwa Mageuzi ya Kiuchumi (HEET) unaofadhiliwa na Benki ya Dunia.

Tukio hili la kihistoria limefanyika tarehe 2 Novemba 2023 ambapo mgeni rasmi alikuwa Mwenyekiti wa Baraza la Chuo Kikuu cha Dar es Salaam Mhe. Balozi Mwanaidi Sinare Maajar.

Balozi Maajar amewataka washauri elekezi na Kitengo cha Usimamizi wa Mradi UDSM kuhakikisha kwamba ujenzi wa majengo hayo unafanyika kitaalamu na kwa kuzingatia kanuni na sheria.

"Baraza la Chuo limejiandaa kufanya ufuatiliaji wa karibu katika utekelezaji wa Mradi huu ambapo utakapokamilika utaongeza ufanisi katika maeneo ya taaluma, utafiti na huduma kwa jamii", amesema Balozi Maajar.

Kwa upande wake Makamu Mkuu wa Chuo Prof. William Anangisye, amesema kwamba lengo la Mradi wa HEET ambapo fedha za ujenzi wa majengo haya zimetoka linaenda sambamba na Dira ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam ya mwaka 2061 na Mpango mkakati wa Chuo wa 2021/2022-2024/2025 unaolenga katika kufanya mageuzi ya kitaasisi yanayoendana na vipaumbele na mahitaji ya taifa ya sasa na ya baadaye.

## *Usimamizi wa Ujenzi wa Mradi*

Kwa mujibu wa Profesa Bernadeta Killian Naibu Makamu Mkuu wa Chuo- Mipango, Fedha na Utawala, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam ambaye pia ni Mratibu wa Mradi wa HEET UDSM, usimamizi wa ujenzi wa mradi huo utafanywa na kampuni mbili ambazo ni M/s Arqes Africa Architects & Interior Designers Limited na M/s Geometry Consultants Limited kwa majengo 10 na 11 mtawalia.

Mkataba baina ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na M/s Arqes Africa Architects & Interior Designers Limited utahusisha usanifu, mapitio na usimamizi wa shughuli za ujenzi katika vitengo mbalimbali Kampasi ya Mwalimu Julius Nyerere Mlimani.

"Vitengo hivyo ni pamoja na Ndaki ya Uhandisi na Teknolojia (CoET) kwa ajili ya ukarabati wa Bloku L,O, na Q; ujenzi wa majengo mapya unaohusisha maabara 7, majengo 5 kwa ajili ya karakana, jengo 1 la mhadhara (wanafunzi 250), madarasa 3 (kila 1 wanafunzi 50) na chumba kimoja cha studio (wanafunzi 50) wa usanifu vitambaa", alisema Prof. Killian.

Majengo mengine katika Kampasi ya Mwalimu Julius Nyarere Mlimani yatakayohusika katika Mradi huu ni Jengo la Taasisi ya Jinsia na Kituo cha Huduma kwa Watu wenye Mahitaji Maalum pamoja na hosteli ya wanafunzi wa uzamili itakayokuwa na uwezo wa kuhudumia wanafunzi 51.

"Katika Ndaki ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (CoICT), Kijitonyama ujenzi utahusisha Jengo 1 la mhadhara (wanafunzi 140); Studio 1 ya maltimidia (wanafunzi 50); maabara 3 za teknolojia ya kisasa (kila 1 wanafunzi 48) na karakana 2 (kila 1 wanafunzi 30)", aliongezea Prof. Killian.

Prof. Killian aliendelea kusema kwamba mkataba wa kwanza utahusisha pia Shule Kuu ya Sayansi Akua na Teknolojia ya Uvuvi (SOAF) eneo la Kunduchi ambapo ujenzi wake unahusisha madarasa 3 ya mhadhara (kila 1 wanafunzi 100) na maabara 1 (wanafunzi 50).




## *Ujenzi wa Majengo IMS – Zanzibar, Ruangwa na Ngongo*

Wakati huhuo Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kimesaini mkataba na Kampuni ya M/s Geometry Consultants Limited kwa ajili ya usanifu, mapitio na usimamizi wa ujenzi wa majengo mapya 11. Majengo hayo ni Jengo la Utawala na majengo mengine ya masuala ya kitaaluma katika Taasisi ya Sayansi za Bahari Buyu Zanzibar (kwa ajili ya vyumba vya mihadhara, maabara, ukumbi wa mikutano na ofisi za walimu na jengo 1 la hosteli litakalokuwa na uwezo wa kuhudumia wanafunzi 80).

Mkataba huu pia utahusisha usimamizi wa majengo ya Ruangwa na Ngongo mkoani Lindi. Kwa upande wa Ngongo ujenzi utahusisha jengo la utawala, vyumba vya mhadhara (wanafunzi 360), jengo la maabara, karakana (vyumba 5) hosteli ya wanaume na hosteli ya wanawake.

"Kwa upande wa Ruangwa ujenzi utahusisha chumba cha mhadhara (wanafunzi 50) na jengo 1 la hosteli litakalohudumia wanafunzi 56 (wanawake 22 na wanaume 34)", alisema Prof. Killian.

Ujenzi wa majengo 21 unaendana na lengo la Maendeleo ya Mradi wa HEET linalohusu kuboresha mazingira ujifunzaji na programu za kipaumbele zinazoendana na mahitaji ya soko la ajira kwa manufaa ya Taasisi za Elimu ya Juu na kuboresha usimamizi wa elimu ya juu nchini Tanzania.

Majengo mengine 3 ambayo yatakamilisha jumla ya majengo 24 ya Mradi wa HEET UDSM na ambayo mkataba wake wa usimamizi utasainiwa baadaye yanahusisha ujenzi wa Kampasi mpya ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam mkoani Kagera. Ujenzi huu utahusisha; Jengo la utawala na masuala ya taaluma; Jengo la kafeteria na masuala ya biashara; na Jengo la Hosteli ya Wasichana.

Kwa ujumla wake Mradi wa HEET UDSM wenye thamani ya Dola za Kimarekani milioni 47.5 unajikita katika maeneo 8 ya msingi. Miongoni mwa maeneo hayo ni i) ujenzi na ukarabati wa miundombinu na kununua vifaa; ii) kufanya mapitio ya mitaala; iii) kukuza utafiti na ubunifu.

Maeneo mengine ni iv) kujenga ushirikiano wa kisekta (za umma na binafsi); v) kuimarisha matumizi ya teknolojia ya dijitali katika ufundishaji; vi) kukuza uwezo wa ndani wa kuzalisha mapato; vii) kuwajengea uwezo wanataaluma na viongozi wa Chuo na Usimamizi, viii) usimassmizi, uratibu, ufuatiliaji na tathmini ya Mradi.

# Kusainiwa kwa Mkataba wa Usimamizi wa Ujenzi wa Majengo ya HEET Chuo Kikuu cha Dar es Salaam



*Mwenyekiti wa Baraza la Chuo Kikuu cha Dar es Salaam*
*Mhe. Balozi Mwanaidi Sinare Maajar*







## ...baadhi ya majengo yatayojengwa...

*Kampasi ya Lindi : Ngongo & Ruangwa*







*Kampasi ya Kagera*



*IMS Buyu Zanzibar*



*SoAF (Kunduchi)*




# Wanufaika wa kundi la kwanza wanaofadhiliwa na Mradi wa HEET Wahitimu

*Na Ally Mambele, UDSM-HEET*




**Bw. Gabriel Mwaijande Paul**
Mhitimu wa Shahada ya Umahiri ya Sayansi katika Uhandisi wa Jiotekniki, Chuo Kikuu cha Leeds, Uingereza



**Bi. Angelina William**
Mhitimu wa Shahada ya Umahiri ya Sayansi katika Sayansi ya Chakula, Chuo Kikuu cha Reading, Uingereza

Kundi la kwanza lenye wafanyakazi wanne wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam walionufaika na ufadhili wa Mradi wa HEET wamehitimu masomo yao ya umahiri.

"Fedha za ufadhili huo ni sehemu za Dola za Kimarekani 200,000 iliyotengwa katika Mradi wa HEET kama mpango wa muda mrefu wa mafunzo na nyingine zilitoka katika bajeti ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Tunafurahi kuwajuza kwamba wanafunzi hawa wanne wamehitimu mafunzo yao kwa ufanisi". Alisema Dkt. Emmanuel Matee, Mtaalamu wa HEET UDSM kwa upande wa kujenga uwezo.

Hawa ni miongoni mwa wafanyakazi kumi waliojisajili katika Programu ya Umahiri chini ya ufadhili wa HEET UDSM. Wafanyakazi hawa wanatoka Ndaki ya Kilimo na Teknolojia ya Chakula pamoja na Ndaki ya Uhandisi na Teknolojia. Wahitimu hao ni Bi. Angelina William Mwakosya, Bi. Salma Damla, Bw. Gabriel Mwaijande Paul na Bi. Mariam Madundo.

Bi. Angelina William, Mkufunzi Msaidizi kutoka Idara Sayansi ya Chakula, CoAF, aliyepata ufadhili Julai 2022 kwa ajili kusoma Digrii ya umahiri katika Sayansi ya Chakula, Chuo Kikuu cha Reading nchini Uingereza ameeleza furaha yake na kutoa shukran za dhati kwa ufadhili aliopatiwa kupitia Mradi wa HEET.

"Nimefanikiwa kupata uzoefu ambao umeimarisha taaluma yangu na kunijengea umahiri katika eneo langu la ubobezi. Kwa hakika ufadhili huu umenipa fursa ya kutangamana na ulimwengu". Amesema Bi. Angelina

Mnufaika mwingine Bi. Salma Damla Mkufunzi Msaidizi kutoka Idara Sayansi ya Chakula, CoAF, amehitimu Digrii ya umahiri katika Sayansi ya Chakula, Chuo Kikuu cha Leeds nchini Uingereza.

"Safari ya masomo yangu ya Digrii ya Umahiri imekuwa na mageuzi makubwa kwangu kitaaluma na kijamii. Msaada wa kifedha na mwongozo ambao nimekuwa nikipata kupitia Mradi wa HEET ni kielezo bora cha kuikamilisha safari yangu ya elimu", amesema Bi. Salma.

Bw. Gabriel Mwaijande Paul, kutoka Idara ya Uhandisi Usafirishaji na Jioteknolojia, CoET pia amekishukuru Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kupitia Mradi wa HEET kwa ufadhili aliopatiwa. Amehitimu Digrii yake ya Umahiri katika Uhandisi Jioknolojia kutoka Chuo Kikuu cha Leeds, nchini Uingereza.

"Kwa kweli ninatambua kwamba nina wajibu wa kutumia maarifa na ujuzi nilioupata kwa manufaa ya jamii yangu na kufanikisha malengo ya Chuo na Mradi na HEET", amesema Bw. Gabriel.

Bi. Mariam Madundo ni mnufaika mwingine wa ufadhili wa HEET kutoka Idara ya Uhandisi Mihimili na Ujenzi, CoET pia alikishukuru Chuo kwa ufadhili alioupata na kuahidi kwamba atatumia maarifa aliyoyapata kwa lengo la kuiendeleza jamii ya Watanzania.




**Dkt. Emmanuel Matee,**
Mtaalamu wa Kujenga uwezo wa Mradi wa HEET, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam

# Kutoka Mezani kwa Naibu Mratibu wa HEET UDSM



## Dkt. Liberato V. Haule

### Naibu Mratibu wa Mradi wa HEET-UDSM

Utekelezaji wa shughuli mbalimbali katika Mradi wa HEET Chuo Kikuu cha Dar es Salaam ulianza mwezi Agosti 2022. Maendeleo ya Mradi yako katika hatua mbalimbali kulingana na muda uliowekwa kwa kila mradi. Mosi, Baadhi ya shughuli, hususani zinazohusu maandalizi, kimsingi zimekwishamalizika na nyingine zinaendelea katika hatua ya utekelezaji. Baadhi ya shughuli zinazohusiana na zabuni kwa wakandarasi zinatarajiwa kukamilika mwishoni mwa Novemba, 2023.

Pili, Kitengo cha Usimamizi wa Mradi wa HEET kilifanya mapitio ya mpango wa utekelezaji na kupendekeza maboresho na marekebisho kadhaa. Mapitio yalizingatia maandalizi ya michoro, mchakato wa upatikanaji wa washauri elekezi kwa ajili ya mapitio ya michoro na usimamizi, na mchakato wa upatikanaji wakandarasi kwa ajili ya ujenzi wa majengo katika maeneo mbalimbali. Kwa ujumla hatua zote hizi zimezingatia tathmini ya uharibifu wa mazingira na athari za kijamii kwa maeneo yote ya mradi.

Tatu, kwa upande wa uboreshaji wa mitaala na kuzingatia mbinu za ubunifu katika ufundishaji, utafiti fuatilizi ulifanyika kwa kuzingatia miongozo iliyoandaliwa. Vitengo mbalimbali vinaendelea kutumia matokeo ya utafiti fuatilizi kuboresha mitaala katika mchakato wa mapitio ya mitaala unaoendelea. Nne, ili kukamilisha shughuli za mradi katika kipengele cha kukuza ushirikiano na sekta binafsi, miongozo mbalimbali imeandaliwa. Miongozo hiyo ni pamoja na mwongozo wa mkataba maalum wa kazi kwa wafanyakazi, mwongozo wa fursa za kazi kwa wafanyakazi na mazoezi kwa vitendo kwa wanafunzi; mwongozo ushirikiano katika shughuli za utafiti na ubunifu na mwongozo wa huduma kwa jamii.

Katika utekelezaji shughuli zinazohusiana na kuimarisha matumizi ya teknolojia ya digitali katika ufundishaji na ujifunzaji pamoja na majukumu mengine ya msingi ya Chuo, Mwongozo wa Kampasi Maizi ya UDSM umeandaliwa. Kwahiyo shughuli zinazohusiana na kipengele hiki zitakuwa zikifanyika kwa kuzingatia mwongozo huu.

Ili kuhakikisha kwamba masuala ya usawa wa kijinsia, elimu jumuishi, na usalama mahali pa kazi yanazingatiwa, kumefanyika mapitio ya sera na nyaraka mbalimbali. Sera hizo ni pamoja na Sera ya Chuo ya kupinga unyanyasaji wa kingono; mapitio ya mkakati wa Chuo kupinga ukatili wa kijinsia; kupinga unyanyasaji na udhalilishaji wa kingono na Elimu kuhusu Afya ya Uzazi na maambukizi ya UKIMWI. Kutokana na mapitio hayo miongozo mbalimbali imeandaliwa. Miongozo hiyo ni pamoja na mwongozo wa Chuo wa utambuzi wa wafanyakazi na wanafunzi wenye mahitaji maalum na mwongozo Chuo wa kushughulikia malalamiko.

Mafanikio ya jumla yaliyopatikana tangu kuanza kwa Mradi Agosti 2022 ni mengi kama yalivyoelezwa katika ujumbe wa Mratibu. Mwaka wa fedha wa 2023/2024 utakuwa muhimu sana katika utekelezaji wa Mradi wa HEET. Kama ilikwishaelezwa hapo awali, mwaka wa kwanza ulijikita zaidi katika kuweka mipango na shughuli za maandalizi zaidi. Mwaka wa pili tutajikita katika kutumia michoro iliyoandaliwa ili kuanza ujenzi pamoja na kumalizia mapitio ya mitaala. Tumejiandaa kukabiliana na changamoto mbalimbali ikiwa ni pamoja na ile ya mrundikano wa shughuli na ununuzi kwa kipindi kimoja ambayo itatokana na mbali na mambo mengine shughuli za ujenzi zitakazofanyika katika maeneo mbalimbali.

Ninatoa shukran za dhati kwa wote waliofanikisha mafanikio hayo. Fedha tulizopata kutoka serikalini kupitia Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia na Wizara ya Fedha zimetusaidia sana katika hatua hii. Msaada wa kitaalamu na miongozo kutoka Benki ya Dunia kupitia kwa kiongozi wa mradi ni wa kutiliwa mfano na wenye manufaa makubwa sana. Tunatoa shukrani za dhati kwa Kitengo cha Chuo kinachosimamia Mradi huu kwa miongozo na ushauri kuhusu mbinu bora za kutekeleza Mradi.

Kwa mara nyingine tena kwa unyenyekevu mkubwa ninawaomba wadau wote waliochangia utekelezaji wa shughuli mbalimbali za Mradi katika mwaka wa kwanza kuendeleza ushirikiano huo katika mwaka wa pili wa utekelezaji wa Mradi.

# *Kikao cha Kamati ya Usimamizi wa Mradi, Oktoba 2023*
















# Tahariri

## Tuungane kwa Pamoja Kukamilisha Mapitio ya Mitaala ya UDSM

Kuanzia Julai 2022 Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kimekuwa katika mchakato wa kina wa mapitio ya mitaala ya shahada za awali na uzamili ili kuendana na miongozo na mipango ya Chuo na Serikali na kwa kuzingatia malengo ya Mradi wa Elimu ya Juu kwa Mageuzi ya Kiuchumi (HEET).

Kama ilivyoripotiwa katika kijarida hiki, tumeshuhudia mafanikio makubwa katika mchakato huu kuanzia hatua ya maandalizi hadi kazi halisi ya mapitio ambapo imeelezwa kwamba kazi hii imekwishafanyika kwa zaidi ya asilimia 80 na inatarajiwa kukamilika mapema mwakani 2024.

Timu ya wapitiaji wa mitaala ilifanikiwa kuandaa miongozo, zana za utafiti fuatilizi zilizofanyiwa majaribio na kufanya mafunzo kwa wanajumuiya walioteuliewa kushiriki katika shughuli hii. Kati ya Novemba 2022 na Machi 2023 watafiti walifanikiwa kukusanya data za utafiti fuatilizi kwa kuwashirikisha watoataarifa 8,000 kati ya matarajio ya watoataarifa 9,111 ambao ni sawa na asilimia 87.8 ya malengo.

Data zilikusanywa kwa njia ya mtandao na nyingine kwa njia ya ana kwa ana hali iliyotoa matokeo thabiti na shirikishi. Hatma ya safari hii ni uchambuzi uliofanywa katika vitengo vya kitaaluma ambao ulijikita katika mambo manne ya msingi ambayo ni umadhubuti, udhaifu, fursa na matishio. Tathmini hii binafsi inaweka msingi wa mapitio ya mitaala kwa kubainisha ubora na maeneo yanayohitaji kuboreshwa kwa kila programu.

Jumla ya programu 200 zilipitiwa kwa kutumia mbinu madhubuti ambazo zinaakisi dhamira ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam katika kuboresha elimu ya juu. Kwa hakika hii ni hatua muhimu sana katika kuzifanyia mabadiliko programu hizi. Mbinu zilizotumika kupata data na mkakati wa kuwashirikisha wabia na wadau mbalimbali vitakisaidia Chuo kuhakikisha kwamba kinaandaa wahitimu watakaokubalika katika soko la ajira.

Mchakato wa upitiaji wa programu ni miongoni mwa majukumu ya kawaida kwa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam ambapo kazi ya kutathmini ubora wa programu za kitaaluma hufanywa kila baada ya miaka kadhaa. Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kinafanya kazi hii kama moja ya majumu yake ya msingi na kama ilivyoelezwa katika dira na rajua, mpango mkakati, sera ya udhibiti ubora pamoja na miongozo ya kitaifa iliyotolewa na Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania.

Ni ukweli usiopingika kwamba mchakato huu siyo tu kwamba utaboresha programu zetu bali utasaidia kuking'arisha Chuo na Taifa kwa ujumla katika uga wa kimataifa. Tunatoa wito kwa wadau wote ikiwa ni pamoja na wanataaluma kutoka katika vitengo vyote vya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kushirikiana katika kuikamilisha safari hii. Ni matumaini yetu kwamba kwa kiasi kubwa proramu zilizoboreshwa zitatoa wahitimu watakaoweza kuendana na mahitaji halisi na mabadiliko yanayotokea ulimwenguni.


HEKIMA NI UHURU

HEET HIGHER EDUCATION FOR ECONOMIC TRANSFORMATION

**Uratibu wa Mradi wa HEET-UDSM**

**Mratibu wa Mradi**
Prof. Bernadeta Killian

**Naibu Mratibu wa Mradi**
Dkt. Liberato V. Haule

**Timu ya Uhariri**

**Mhariri Mkuu &**
**Mtaalamu wa Uhusiano kwa Umma na Mawasiliano HEET-UDSM**
Dkt. Dotto Paul Kuhenga

**Wahariri**
Dkt. Lupa Ramadhani (Kiingereza)
Dkt. Mussa Hans (Kiswahili)

**Waandishi:**
Jackson Isdory
Zamda George
Ally Mambele
Mercy Machange
Remmy Wilson

**Mpigapicha:**
Tumaini Kibangala

**Msanifu**
Michael Mwakatobe



# Matukio katika Picha





*Taasisi ya Taaluma za Jinsia wakiendesha warsha na wadau kujadili mitaala, tarehe 16 Juni, 2023*



*Mkurugenzi wa Rasilimaliwatu na Utawala, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Bi. Asha Hayeshi akiongea na washiriki wa Warsha ya Maafisa Rasilimaliwatu na Utawala wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam iliyofanyika Kibaha tarehe 2 Oktoba 2023*




*Washiriki wa Warsha ya Maafisa Rasilimaliwatu na Utawala wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kuhusu kushughulikia malalamiko yanayohusu mradi wa HEET. Warsha hii ilifanyika tarehe 2 Oktoba 2023*



*Dkt. Paul Ndumbaro, Ujenzi*

*CPA. Ally Mringo, Fedha*

*Dkt. Jackline Mgumia, Jamii*

*Dkt. Innocent Pantaleo, Ufuatiliaji & Tathmini*

*Naibu Mratibu wa Mradi wa HEET -UDSM Dkt. Liberato Haule (kushoto) akiwatambulisha wajumbe wa timu ya utekelezaji wa mradi huo Chuo Kikuu cha Dar es Salaam*





*Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda akiongea na viongozi na wakazi wa mkoa wa Lindi kuhusu kuanzishwa Kampasi mpya ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam mkoani Lindi*



*Bw. Bakari Machumu,Afisa Mtendaji Mkuu, wa Kampuni ya Mwananchi Communications Ltd akichangia hoja katika Mkutano mmojawapo wa Kamati za Ushauri za Kisekta*



*Moja ya Vikao vya Kamati za Ushauri za Kisekta*





*Baadhi ya Wajumbe wa Kamati ya Utekelezaji wa Mradi wa HEET, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam katika moja ya mikutano ya mradi*




*Bw. Job Semboja Mtaalamu wa Manunuzi, HEET-UDSM*



*Dkt. Mohammed K. Maalim Mtaalamu kutoka IMS - Zanzibar, HEET-UDSM*

*Dkt. Fatuma Simba Mtaalamu wa Ushirikiano na Tasnia, HEET-UDSM*




*Dkt. Edmund Mabhuye Mtaalamu wa Mazingira, HEET-UDSM*






*Prof. Bernadeta Killian,*
*Naibu Makamu Mkuu wa Chuo-Mipango,*
*Fedha na Utawala, UDSM*

# Maafisa Rasilimaliwatu UDSM wajengewa uwezo wa namna ya kushughulikia malalamiko

*Na Zamda George, UDSM-HEET*

Naibu Makamu Mkuu wa Chuo-Mipango, Fedha na Utawala, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam Prof. Bernadeta Killian amewataka maafisa rasilimaliwatu kufanya kazi kwa weledi ikiwa ni pamoja na kushughulikia malalamiko ya wafanyakazi na wadau wengine.

Prof. Killian ambaye pia ni mratibu wa HEET - UDSM aliyasema hayo katika warsha kwa maafisa rasilimaliwatu na utawala kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam iliyofanyika hivi karibuni katika Shule Kuu ya Uongozi ya Mwalimu Nyerere iliyopo Kibaha, mkoani Pwani.

“Tumekutana hapa ili kukumbushana kuhusiana na majukumu yetu ya kiutawala na wajibu wetu unaohusisha mbali na mambo mengine kushughulikia malalamiko mbalimbali ikiwa ni pamoja na yale yanaohusiana na Mradi wa HEET”, amesema Prof. Killian.

Prof. Killian ameeleza pia kuhusu mageuzi ya ugatuzi wa madaraka kwa baadhi ya majukumu ya kiutawala ambayo yamekuwa yakifanyika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na umuhimu wa maafisa hao katika kufanikisha majukumu hayo.

“Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kimeamua kugatua madaraka kwenda katika vitengo mbalimbali kwa baadhi ya majukumu ambayo awali yalikuwa yakifanywa katika ngazi ya juu ya utawala lengo likiwa ni kuongeza ufanisi na uwajibikaji”, amesisitiza Prof. Killian.

Warsha ilihusisha mada mbalimbali muhimu zilizotolewa katika mfumo wa uwasilishaji na mjadala ukijikita zaidi katika Mradi wa HEET UDSM na utaratibu wa kushughulikia malalamiko. Wataalamu kutoka timu ya HEET UDSM walishiriki katika warsha hii na kushirikiana katika kujibu maswali ya washiriki wa warsha.

Dkt. Edmund Mabhuye, Mtaalamu wa masuala ya mazingira aliwasilisha madondoo kuhusu Mradi wa HEET UDSM akiangazia zaidi katika malengo na umuhimu. Dkt. Jackline Mgumia ambaye ni mtaalamu wa masuala ya kijamii alishiriki katika mjadala akitoa ufafanuzi kuhusiana na utaratibu wa kushughulikia malalamiko.

Wakati huo huo Bi. Asha Hayeshi, Mkurugenzi, Rasilimaliwatu na Utawala, alisisitiza umuhimu wa warsha hiyo katika kujenga ushirikiano na ufanisi kwa washiriki watakaporejea kwenye kituo chao cha kazi.

“Warsha hii ni hatua muhimu katika kuhakikisha kwamba malalamiko yanayohusiana na Mradi wa HEET yanashughulikiwa ipasavyo na kwa ufanisi. Tunathamini mchango wa wafanyakazi wetu na wadau na tumejipanga kuhakikisha kwamba changamoto zao zinasikika na kutatuliwa”, amesema Bi. Hayeshi.


Washiriki wa warsha pia walinufaika kutokana na wasilisho kuhusu mradi wa HEET lililotolewa na Dkt. Liberato Haule, Naibu Mratibu wa Mradi wa HEET UDSM. Dkt. Haule amewataka washiriki kuzingatia kupata mageuzi yenye tija na mikakati ya kushughulikia malalamiko ili kuhakikisha kuwa mradi unakuwa na mafanikio.

# Maafisa Mawasiliano Wakubaliana Mkakati wa Kutangaza Mradi wa HEET

***Na Remmy Wilson, UDSM-HEET***



*Dkt. Dotto P. Kuhenga, Mtaalamu wa Mawasiliano na Uhusiano kwa Umma HEET-UDSM.*



*Washiriki wa Warsha ya Maafisa Uhusiano kwa Umma na Mawasiliano kutoka katika taasisi mbalimbali za elimu ya juu zinazotekeleza Mradi wa HEET iliyofanyika Jijini Mwanza mwezi Julai 2023.*

Maafisa Uhusiano kwa Umma na Mawasiliano kutoka katika taasisi mbalimbali za elimu ya juu zinazotekeleza Mradi wa Elimu ya Juu kwa Mabadiliko ya Kiuchumi (HEET) wamefanya mkutano hivi karibuni jijini Mwanza na kuweka mikakati ya namna ya kupata na kusambaza taarifa kuhusu mradi huu kwa jamii.

Mkutano huo wa siku tano, ulioratibiwa na Kitengo cha Mawasiliano na Taarifa kutoka Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, ulifanyika mwezi Julai 2023 katika hoteli ya Adden Jijini Mwanza na kuwashirikisha zaidi ya washiriki 25 ambao walipata fursa ya kujadili na kuweka mipango kadhaa ikiwa ni pamoja na mikakati ya kitaasisi ya kutangaza Mradi wa HEET kwa umma.

Bi. Sylivia Lupembe ambaye ni Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano na Taarifa kutoka Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia alifafanua malengo ya Mradi wa HEET na kusisitiza nafasi ya maafisa hao katika kufanikisha mikakati ya mawasiliano na taarifa zinazohusiana na Mradi wa HEET.

"Ni muhimu sana kwa maafisa mawasiliano kuwa na welewa wa kutosha na kuhusika kikamilifu katika hatua mbalimbali za mradi. Ninatoa wito kwenu nyote kujenga ufahamu katika michakato yote ya mradi na kusambaza taarifa za mradi kikamilifu na kwa wakati kwa wadau wa nje na ndani", amesema Bi. Lupembe.

Amesisitiza kwamba maafisa mawasiliano wanapaswa kusoma na kufahamu nyaraka zote za msingi zinazochukuliwa kuwa ni mhimili wa uendeshaji wa mradi na maeneo ya msingi ya kuripotiwa ambayo ni Waraka wa Uidhinishaji wa Mradi na Chati ya Malengo ya Mradi.


Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM) kilishiriki kikamilifu katika mkutano huu ambapo mtaalamu wa mawasiliano wa HEET-UDSM Dkt. Dotto Paul Kuhenga aliwaongoza washiriki katika mjadala kuhusu mchakato na njia za kuandaa mkakati wa mawasiliano kuhusiana na Mradi wa HEET katika Taasisi zao ambao utaongeza welewa, ushiriki wa jamii, na kuutangaza mradi.

Dkt. Kuhenga aliwaongoza washiriki hatua kwa hatua namna ya kuandaa mkakati madhubuti na wenye mafanikio kwa ajili ya utekelezaji pamoja na mbinu mbalimbali zitakazotumika katika kukabiliana na changamoto zinazoweza kuwakabili maafisa mawasiliano katika kufanikisha mawasiliano katika Mradi wa HEET.

"Mkakati wa mawasiliano ni mwongozo wa msingi na dira itakayokuwezesha kubaini hali ya mawasiliano taasisini na hususani mawasiliano yanayohusiana na Mradi wa HEET, na kukuongoza katika kutafuta rasilimali na kutumia zana na mikakati muafaka katika kutoa taarifa zinazohusiana na shughuli za mradi ndani na nje ya jamii", amesema Dkt. Kuhenga.

Washiriki walionesha utayari wao katika kuandaa mkakati wa mawasiliano wenye tija kuhusiana na Mradi wa HEET katika taasisi zao kutokana na mafunzo waliyoyapata kutokana na wasilisho la Dkt. Kuhenga.

Mbali na Dkt. Dotto Kuhenga, maafisa wengine wa mawasiliano kutoka UDSM walioshiriki mkutano huu ni pamoja na Bw. Remmy Wilson kutoka Kampasi ya Mwalimu Nyerere-Mlimani, Dkt. Ponsiano Kanijo na Bi. Johari Buliro kutoka Chuo Kishiriki cha Elimu Mkwawa (MUCE) pamoja na Dkt. Lameck E. Mpalanzi kutoka Chuo Kishiriki cha Elimu Dar es Salaam (DUCE).



*Kutoka Kushoto: Bw. Remmy Wilson(Kampasi ya Mlimani-UDSM), Bi. Johari Buliro (MUCE), Dkt. Dotto Kuhenga (Kampasi ya Mlimani-UDSM), Dkt. Lameck E. Mpalanzi (DUCE) na Dkt. Ponsiano Kanijo (MUCE).*

# UDSM Yapokea Magari na Vifaa vya TEHAMA Kuboresha Ufundishaji na Ujifunzaji kwa Wanafunzi wenye Mahitaji Maalum

*Na Mercy Machange, UDSM-HEET*





*Mratibu wa Mradi wa UDSM-HEET Prof. Bernadeta Killian (wa pili kushoto) na Mkurugenzi wa Mipango, Maendeleo na Uwekezaji, Prof. Siasa Mzenzi wakishika mfano wa ufunguo wa gari kuashiria kupokea magari matatu aina ya Toyota Land Cruiser kwa ajili kusaidia shughuli za elimu na taaluma Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Wengine wanaoshuhudia ni Kaimu Naibu Makamu Mkuu wa Chuo-Utafiti, Prof. Nelson Boniface (katikati), Naibu Mratibu wa Mradi wa HEET-UDSM, Dkt. Liberato Haule na wafanyakazi wengine wa Chuo.*

Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kimepokea Kompyuta, vifaa vya maabara na magari matatu aina ya Toyota Land Cruiser kuwezesha ufundishaji na ujifunzaji kwa wanafunzi wenye mahitaji maalum.

Katika makabidhiano hayo yaliyofanyika hivi karibuni katika Shule Kuu ya Elimu Prof. Bernadeta Killian Naibu Makamu Mkuu wa Chuo- Mipango, Fedha na Utawala ambaye pia ni Mratibu wa Mradi wa HEET-UDSM amesema kwamba magari na vifaa hivi ni zana muhimu katika utekelezaji wa majukumu ya Chuo kwa kuzingatia dhamira yake katika utoaji wa elimu jumuishi.

"Vifaa hivi vitawasaidia wanafunzi wetu wenye mahitaji maalum. Vitaimarisha Kituo cha Huduma kwa watu wenye mahitaji maalum ikiwa ni sehemu ya dhamira yetu ya kuhakikisha kwamba tunazingatia usawa katika ujifunzaji na mazingira rafiki ya kazi kwa wafanyakazi na kujisomea kwa wanafunzi wenye mahitaji maalum", amesema Prof. Killian.

Prof. Killian alieleza zaidi kwamba vifaa hivi vya kisasa vilivyopokelewa siyo tu kwamba vitaboresha mazingira yao ya ujifunzaji bali pia vitasaidia kuwaunganisha na wenzao na watoa huduma.

"Magari haya matatu yatasaidia kukamilisha majukumu mbalimbali ya mradi. Tunatoa shukrani zetu za dhati kwa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia na Serikali kwa ujumla kwa kukihusisha Chuo chetu katika Mradi huu", amesisitiza Prof. Killian.

Dkt. Aurelia Kimaro, ambaye alimwakilisha Meneja wa Kituo cha Huduma kwa Watu wenye Mahitaji Maalum, Dkt. Sarah Kisanga alionesha furaha yake na kushukuru kwa vifaa vilivyotolewa.

"Leo ni siku ya furaha kwetu tukiwa tunapokea vifaa hivi ambavyo vitasaidia kwa kiasi kikubwa katika kuleta maendeleo endelevu kwa wanafunzi wetu wenye mahitaji maalum", amesema Dkt. Kimaro.

"Tunaamini katika elimu jumuishi ambapo kila mwanafunzi ana haki sawa ya kujifunza. Ulemavu daima haupaswi kuwa kikwazo kwa mtu kujiendeleza. Tunatoa shukran zetu za dhati kwa menejimenti ya Chuo na Mradi wa HEET kwa kuona umuhimu wa elimu jumuishi na kutupatia rasilimali hizi", amesema Dkt. Kimaro.

Mratibu wa Kituo cha Huduma kwa Watu wenye Mahitaji Maalum, Jerome Mbogo amesisitiza katika athari ya mageuzi yatakayotokana na rasilimali hizi " rasilimali hizi zitaleta mabadiliko makubwa katika mkabala wetu wa elimu jumuishi na zitakuwa ni zana muhimu zitakazowasaidia wanafunzi wenye mahitaji maalum na kuimarisha upatikanaji wa mazingira ya elimu jumuishi".

Wanafunzi katika Kituo hiki pia wamejawa na furaha kushuhudia upatikanaji wa rasilimali hizi na wanaamini kwamba zitawanufaisha katika safari yao na kuwasaidia kufikia malengo waliyojiwekea.

Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kimedhamiria kuendelea kujenga mazingira ya elimu jumuishi. Mradi huu wa HEET umekuja kwa wakati na msisitizo wake ukiwa katika elimu jumuishi na kuhakikisha kwamba wanafunzi wote wana fursa sawa bila kujali mahitaji yao binafsi na ushirikishwaji kwa siku za baadaye.



# UDSM yaanzisha Ofisi ya Ushirikiano baina ya Chuo na Waajiri

*Na Zamda George, UDSM-HEET*

Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kimeanzisha Ofisi ya Ushirikiano baina ya Chuo na Waajiri ndani ya Kurugenzi ya Huduma kwa Umma ikiwa ni sehemu ya utekelezaji malengo wa Mradi wa Elimu ya Juu kwa Mageuzi ya Kiuchumi (HEET).

Ofisi hii ya ushirikiano itafanya kazi ya kuchochea ushirikiano baina ya Chuo na wadau mbalimbali. Kazi yake ya msingi ni kuhakikisha kwamba huduma zinazotolewa Chuoni zinaendana na mahitaji ya soko la ajira na hivyo kuchangia katika ajenda ya kitaifa kujenga Tanzania ya Viwanda.

Kwa mujibu wa Ofisa wa ofisi hii Dkt. Eva Shayo, ofisi yake itakuwa ikifanya mambo mbalimbali kufikia malengo yake ikiwa ni pamoja na kuwezesha kupatikana kwa ujuzi kwa kutafuta fursa kwa wafanyakazi na wanafunzi katika programu za mazoezi kwa vitendo, ajira za mikataba maalum na ukurufunzi kwa wahitimu.

"Ofisi hii pia itahusisha wataalamu wa nje kwa njia ya kuratibu na kuwezesha ushirikishwaji wa wataalamu hao kwa lengo la kujenga ubobezi wa kitaaluma. Aidha, tutasimamia Kamati za Ushauri kwa kuziwezesha kufanikisha majukumu yake na kuhakikisha kwamba zinashiriki kikamilifu katika uboreshaji wa mitaala na utafiti", amesema Dkt. Shayo.

Dkt. Shayo anaeleza kwamba ofisi hii pia itaratibu mijadala baina ya Chuo na waajiri kwa lengo la kutoa uwanja wa ubadilishanaji wa maarifa na ushirikiano na wakati huohuo kuimarisha ubia na waajiri pamoja na taasisi mbalimbali na hatimaye kutoa fursa kwa ajili ya shughuli za utafiti na ubunifu.

"Katika kukuza ubobezi, tutasadia ushirikishwaji wa wafanyakazi wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam katika vitengo vya kitaalamu na kuwasaidia katika kukuza ujuzi wao na kujenga mtandao", amesema Dkt. Shayo.



***Dkt. Eva Shayo***
***Ofisa,***
***Ofisi ya Ushirikiano baina ya chuo na Tasnia***



*CPA Dkt. Merezia Wilson (kushoto) wa Shule Kuu ya Biashara Chuo Kikuu cha Dar es Salaam akiwa katika program ya mafunzo maalum ya wafanyakazi katika Kampuni ya Claritas International. Kushoto kwake ni mkurugrenzi mwenza wa Claritas International , ACPA-PPP Chrisant Christopher Bantulaki*



*Mhandisi Dkt. Aviti Mushi (kushoto) na Mhandisi Dkt. Ngessa Ezekiel (kulia), Wote kutoka Ndaki ya Uhandisi na Teknolojia, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam wakiwa katika program ya mafunzo maalum ya wafanyakazi, kwa miezi miwili, katika kampuni ya Super Group Ltd, Dares Salaam. Katikati ni Mwenyekiti na mkurugenzi Mtendaji wa Super Group Ltd, Bw. Seif Seif*

Aidha, Dkt. Shayo anaeleza kwamba miongoni mwa mafanikio ambayo ofisi yake imetekeleza ni kusainiwa kwa Mkataba wa Maridhiano baina ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na makampuni mbalimbali ikiwa ni pamoja na Super Group Limited ambapo imekuwa mwanzo wa fursa kwa baadhi ya wanataaluma.

"Hivi sasa tunafurahi kuwaeleza kwamba kutokana na ushirikiano huu wahadhiri wawili wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam Mhandisi Dkt. Aviti Mushi na Mhandisi Dkt. Ngessa Ezekiel kutoka Idara ya Uhandisi Umeme, Ndaki ya Uhandisi na Teknolojia wamepata mkataba maalum kama wahandisi umeme katika kampuni ya Super Group Limited", amesema Dkt Shayo.

Ubia huu ni mfano thabiti wa ushirikiano baina ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na Super Group Limited utakaosaidia kukuza vipaji na kuzifanya programu zetu kuendana na mahitaji halisi ya soko la ajira. Fursa hii siyo tu itawanufaisha wahandisi hao bali pia ina faida endelevu kwa UDSM na Super Group Limited.

Anaendelea kueleza kwamba mkataba huu utawasaidia kujenga uzoefu katika mazingira halisi na kukuza stadi na ufanisi katika majukumu yao ya uhandisi umeme na hatimaye kuwanufaisha pia wanafunzi wanaowafundisha na kuwasimamia. Watahusika moja kwa moja katika usanifu, matumizi na uboreshaji wa vifaa vya umeme na mifumo katika kampuni ya Super Group Limited na kuchangia katika ukuaji wa Kampuni na ufanisi katika utendaji.

Kwa upande wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, mkataba huu unaonesha dhamira ya dhati ya Chuo katika kutoa wahitimu wanaokubalika katika soko la ajira. Unaimarisha ushirikiano baina ya Chuo na ulimwengu wenye ushindani kuhakikisha kwamba programu za kitaaluma zinazofundishwa zinaendana na mahitaji ya soko la ajira.

Kwa upande wa Super Group Limited, Ushirikiano huu unatoa fursa ya kuunganisha maarifa ya kitaaluma na uwezo wa kitafiti. Unawawezesha kutumia utaalamu na ujuzi kutoka kwa wanajumuiya wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kuchangia katika uboreshaji wa utendaji kazi halisi.

"Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kinaipongeza Super Group Limited kwa utayari wake katika kujenga ushirikiano baina ya Chuo na soko halisi la ajira. Kwa pamoja tunajenga mustakabali imara ambapo taaluma zinazofundishwa chuoni na mazingira halisi ya kazi vinawekwa pamoja kupata mafanikio yanayotarajiwa", amesema Dkt. Shayo.





# Waratibu Wapewa Mafunzo kuhusu Usimamizi wa Vituo vya Uatamizi na Ubunifu

*Na Ally Mambele, UDSM-HEET*

Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kupitia Kurugenzi ya Ubunifu na Ujasiriamali kimeendesha mafunzo kwa waratibu wa ubunifu na ujasiriamali kutoka katika vitengo vyote vya kitaaluma Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kwa lengo la kuwapa stadi ya namna ya kusimamia vituo vya uatamizi na ubunifu.

Mafunzo hayo ya siku tatu yaliyofanyika kuanzia tarehe 23 hadi 25 Agosti, 2023 ni sehemu ya mfululizo wa mafunzo 10 ya muda mfupi ambayo yataendeshwa katika vitengo mbalimbali ndani ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam ili kuwawezesha wafanyakazi wenye ujuzi wa kisasa na kiubunifu kusaidia kuboresha nyanja za ufundishaji, ujifunzaji na utafiti.

Aidha, mafunzo yatasaidia katika uboreshaji wa mitaala na wakati huohuo kujenga uwezo ikiwa ni utekelezaji wa sehemu ya majukumu ya mradi.

Mkurugenzi wa Utafiti na Machapisho Dkt. Mussa Mgwatu ambaye alimwakilisha Kaimu Naibu Makamu Mkuu wa Chuo-Utafiti, Prof. Nelson Boniface katika ufunguzi wa mafunzo hayo aliwaeleza washiriki wa mafunzo kwamba wana jukumu la kutumia fursa hii adhimu katika kuweka msingi siyo tu kwa mustakabali wa wanafunzi bali pia kwa uwanja mpana wa ubunifu ndani ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

“Programu hii ya mafunzo imeandaliwa kwa lengo kuwapatia waratibu kutoka katika vitengo mbalimbali mikakati na zana za kusimamia programu za uatamizi katika vitengo vyao. Programu hii itakuwa ni msingi wa kuibua mawazo na kuyatumia katika utatuzi wa maisha halisi ya jamii”, amesema Dkt. Mgwatu.

Wakati wa mafunzo hayo ya siku tatu washiriki wa mafunzo walipata fursa ya kufanya ziara ya kutembelea kituo cha uatamizi kutoka katika Ndaki ya Habari na Mawasiliano, Tume ya Sayansi na Teknolojia na Nafasi Arts Space lengo ikiwa ni kujifunza mchakato wa kuanzisha vituo vya uatamizi katika vitengo vyao kuanzia kwenye wazo hadi kuwa na kitu halisi.

Ziara hii iliwafungua macho waratibu hao na kuwa kichocheo katika kuanzisha vituo vya uatamizi katika vitengo vyao. “Tunaamini kwamba maarifa na ujuzi tulioupata katika ziara hii vitakuwa na msaada mkubwa katika mchakato wa kuanzisha na kusimamia vituo vya uatamizi katika vitengo vyetu”. Amesema Bw. Damas Kamala kutoka Shule Kuu ya Uandishi wa Habari na Mawasiliano kwa Umma.








**Prof. Nelson Boniface**
Kaimu Naibu Makamu Mkuu wa Chuo-Utafiti



## Mafunzo kwa Waratibu wa Milikidhihini Chuo Kikuu cha Dar es Salaam

Kwa upande mwingine hivi karibuni Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kupitia Ofisi ya Milikidhihini kiliendesha programu ya mafunzo kuhusiana na milikidhihini kwa waratibu wa milikidhihini kutoka katika Ndaki, Shule kuu, Taasisi na Idara kuu za Chuo Kikuu.

Mafunzo haya, yakiwa sehemu ya Programu ambayo imefadhiliwa na Mradi wa HEET UDSM, yalilenga kuwapa washiriki maarifa na ujuzi unaohitajika kulinda milikidhihini na kukuza ubunifu na ujasiriamali ndani ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Mafunzo yalihusisha mada mbalimbali zinazohusiana na haki ya milikidhihini, ikiwa ni pamoja na hakimiliki, majina ya biashara, na siri za biashara. Aidha, washiriki walipatiwa elimu kuhusu sheria za milikidhihini na utaratibu wa kusajili na kusimamia haki za milikidhihini Tanzania.

# UDSM, TPSF na Watendaji Wakuu Wafanya Mdahalo Kuhusu Wahitimu na Soko la Ajira

*Na Jackson Isdory, UDSM-HEET*




*Afisa Mtendaji Mkuu wa Benki ya CRDB, Bw. AbdulMajid Mussa Nsekela (wa tatu kushoto) akizungumza wakati wa mdahalo wa kimkakati wa Ushirikiano baina ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na Makampuni uliofanyika katika Hoteli ya Serena, Dar es Salaam tarehe 11 Julai, 2023. Wazungumzaji wengine (pichani) ni pamoja na Mtendaji Mkuu wa Helium Gas, Bw. Fidelis Lekule (wa tatu kulia), Mkurugenzi Mtendaji wa Multichoice Tanzania Ltd, Bi. Jacqueline Woiso (wa pili kushoto), Meneja wa Biashara wa Tanzania Horticultural Association (TAHA), Bw. Kelvin Remen (wa pili kulia) na Msimamizi Mwenza Kitaifa, Tanzania Deloitte East Africa, Bw. David Nchimbi (wa kwanza kushoto). Mwongozaji wa Mdahalo huu alikuwa Dkt. Fatuma Simba (wa kwanza kulia), Mtaalamu wa Ushirikiano na Tasnia, katika Mradi wa HEET-UDSM*

Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kwa kushirikiana na Taasisi ya Sekta Binafsi Tanzania imefanya Mdahalo wa Kimkakati na kihistoria na watendaji wakuu wa makampuni tarehe 11 Julai 2023 jijini Dar es Salaam. Lengo la mdahalo huu ni kukiwezesha Chuo kuandaa wahitimu wanaoajirika na kuwa na manufaa katika sekta binafsi na sekta ya umma.

Mdahalo huu uliolenga kuimarisha ushirikiano baina ya Chuo na sekta ya ajira (binafsi na za umma) kwa kuwaandaa wahitimu wanaoajirika na watakaokuwa na manufaa katika soko la ajira ulifunguliwa na Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Zanzibar, Mhe. Jamal Kassim Ali (MB) ambaye amesisitiza umuhimu wa ushirikiano baina ya maarifa yanayotolewa na soko la ajira.

"Sekta binafsi ni mhimili muhimu wa uchumi wetu na vyuo vyetu vinapaswa kutoa rasilimaliwatu yenye ubora utakaosaidia katika ukuaji wa sekta hii", amesema Mhe. Ali.

Amesisitiza kwamba mahitaji ya kuwianisha maarifa na stadi baina ya taaluma inayotolewa na sekta binafsi yanazingatia na kwamba wahitimu watakaoandaliwa kwa kupewa ujuzi unaohitajika watakuwa na mchango mkubwa katika soko la ajira.

Mhe. Waziri pia amekipongeza Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kwa kuandaa mdahalo huo ambao umekuwa ni jukwaa muhimu la kujadili namna ambavyo programu za Chuo zinaweza kuandaliwa kwa kuzingatia mahitaji ya soko la ajira.

## Ushirikiano katika kuziba pengo baina ya maarifa na mahitaji ya soko la ajira

Prof. William A. L. Anangisye, Makamu Mkuu wa Chuo, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam ameonesha matumaini yake kwa washiriki wa mdahalo huo na kusisitiza umuhimu wa ushirikiano baina ya Chuo na waajiri katika kuandaa wahitimu wanaoajirika.

Prof. Anangisye anasisitiza dhamira ya Chuo katika kujenga Taasisi na kuimarisha ushirikiano baina yake na sekta ya ajira hususani sekta binafsi kwa lengo la kubainisha mahitaji ya soko la ajira na ujuzi unaohitajika.

"Mdahalo huu utakisaidia Chuo wakati wa mapitio ya mitaala ili kuwa na programu zinazoendana na mahitaji yenu halisi na kuziba pengo lililopo la ujuzi na maarifa", amesema Prof. Anangisye.

Mada kuu katika mdahalo huu ilikuwa "Kuwezesha kupatikana kwa wahitimu wanaoajirika kwa matokeo bora katika jamii". Mdahalo uliwahusisha washiriki maarufu kutoka katika sekta mbalimbali ambao kwa kiasi kikubwa watakisaidia Chuo kushirikiana na wadau na kukuza ushirikiano na sekta za umma na sekta binafsi.

Mtendaji Mkuu wa TPSF Bw. Raphael Maganga alisema kwamba mdahalo huu ni fursa muhimu ya kubadilishana uzoefu na kukuza ushirikiano kwa kuzingatia kwamba Mapinduzi ya Nne ya Viwanda yanasisitiza suala la ubia.

Katika mdahalo huu Prof. Goodluck Urassa kutoka Shule Kuu ya Biashara aliwasilisha mada inayohusu changamoto, pengo na mapendekezo ya namna ya kuwa na maarifa yatakayotoa wahitimu wanaoajirika.

## Mafanikio ya Mdahalo

Katika mdahalo huu tumeshuhudia mjadala mpana miongoni mwa washiriki wakibadilishana mawazo na kubainisha fursa za ushirikiano baina ya taaluma na mahitaji halisi ya soko la ajira na hivyo kuwapatia wanafunzi ujuzi na maarifa yanayohitajika watakapoajiriwa.

Washiriki waliohudhuria mdahalo huo walifurahi kuona jitihada ambazo Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kimezichukua ili kuziba pengo lililopo baina ya taaluma inayofundishwa na mahitaji halisi ya soko la ajira.

Hakuna shaka kwamba mdahalo huu wa kimkakati utawanufaisha kwa pamoja wanafunzi na sekta binafsi, kukuza ubunifu na kuwaandaa wahitimu kulingana na mahitaji ya soko la ajira", mmoja wa Watendaji wakuu alisema.

Mdahalo huu ulikuwa ni sehemu ya utekelezaji wa moja ya malengo ya Mradi wa Elimu ya Juu kwa Mageuzi ya Kiuchumi, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (HEET UDSM). Katika muktadha huu Mradi unalenga kuboresha mazingira ya ujifunzaji, kuwianisha programu za kipaumbele na mahitaji ya soko la ajira na kuboresha usimamizi wa Taasisi za Elimu ya Juu.




Dkt. Ibwe Kwame, Mtaalamu wa Mfumo wa Dijitali, katika Mradi wa HEET, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam



Vifaa vipya vya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano vikipokelewa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.



Dkt. Mussa Kissaka, Mkurugenzi, Teknolojia ya Habari na Mawasiliano

# Miundombinu ya Mtandao UDSM Kuboreshwa ili Kuimarisha Mawasiliano ya Dijitali

*Na Remmy Wilson, UDSM-HEET*

Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kinafanya uboreshaji mkubwa wa miundombinu yake ya mtandao kwa lengo la kuhakikisha kwamba mtandao unapatikana kwa ubora na uhakika.

Habari hii njema imetolewa na Dkt. Kwame Salum Ibwe Mtaalamu wa HEET UDSM kwa upande wa maendeleo ya mfumo wa dijitali.

"Uboreshaji unafanywa kwa kusuka upya kwa kiasi kikubwa mfumo wote wa mtandao na hivi sasa mzabuni amekwishapewa mkataba wa kuimarisha miundombinu ya mtandao ambapo utakapokamilika utasaidia kuimarisha mtandao wa mawasiliano na hivyo kuwezesha upatikanaji wa uhakika wa mfumo wa mawasiliano ya dijitali ndani ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam", amesema Dkt. Ibwe

Dkt. Ibwe ameeleza kwamba uboreshaji huu utahusisha mifumo mbalimbali iliyojengwa ili kukuza uwezo wa Chuo katika mifumo ya kiteknolojia. Ameeleza kwamba uimarishaji wa mtandao hadi kufikia Gbps 10 (Gigabits 10 kwa sekunde) utakuwa na faida lukuki ikiwa ni pamoja na kuimarisha mfumo wa kusafirisha data na uunganishaji wa mtandao kwa ujumla.

"Kuongezeka kwa kipimo cha data kuna faida mbalimbali ikiwa ni pamoja na kuimarisha spidi ya kuhamisha data, kuwa na uwezo wa kutuma na kupokea video zenye ubora na kuokoa muda", amefafanua Dkt. Ibwe.

Aidha, amesema kwamba uboreshaji wa mtandao ni miongoni mwa vipengele muhimu katika majukumu yanayofanywa chini ya Mradi wa HEET ambayo yanahusisha kuwa na Kampasi Maizi (Smart Campus) ili kuendana na mahitaji ya sasa ya elimu ya juu katika ulimwengu wa dijitali.

Kuhusiana na utekelezaji wa malengo ya Mradi wa HEET, Dkt. Ibwe amesema kwamba kipengele cha TEHAMA kinahusisha shughuli mbalimbali zinazolenga kuimarisha mfumo wa dijitali ndani ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Shughuli hizo ni pamoja na usawazishaji wa mfumo wa wazi wa hifadhi ya masuala ya elimu; uimarishaji wa mfumo wa majarida mkondoni na uboreshaji wa mfumo wa baruapepe za UDSM.

Wakati huo huo wafanyakazi wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam wameonesha shauku yao katika mchakato huu wa uboreshaji wa miundombinu ya mtandao na kubainisha manufaa yakayopatikana kutokana hatua hii katika majukumu yao ya kila siku na shughuli za utafiti.

"Hakuna shaka kwamba uboreshaji huu wa mtandao utaongeza ufanisi katika kazi zetu na kutupatia fursa zaidi ya kupata nyaraka zilizo katika mfumo wa dijitali", amesema mmoja wa wafanyakazi

Maeneo mengine yanayohusiana na miundombinu ya mtandao ni pamoja na uimarishaji wa mfumo wa usalama wa kimtandao na teknolojia kwa ajili ya masuala ya utafiti. Mambo yote haya yanafanyika kuhakikisha kwamba Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kinaendelea kuwa mstari wa mbele katika mabadiliko ya kiteknolojia na usambazaji wa maarifa.

Wanajumuiya ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam wanasubiri kwa hamu kukamilika kwa mradi huu wakitarajia mapinduzi katika shughuli zao za kitaaluma na utafiti.

# Sera na Miongozo Mbalimbali Vyaandaliwa UDSM

*Na Mercy Machange, UDSM-HEET*

Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM) kimeanza mchakato wa kushughulikia malalamiko, ukatili wa kijinsia na unyanyasaji wa kingono kwa kuandaa sera na miongozo mipya na kufanyia mapitio ile iliyokuwepo. Kazi hii imefanyika kwa ufadhili wa Mradi wa Elimu ya Juu kwa Mageuzi ya Kiuchumi, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (HEET- UDSM).

Akielezea kuhusu suala hili Dkt. Lulu Mahai ambaye ni Mkurugenzi wa Taasisi ya Taaluma za Jinsia Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na Mratibu wa Masuala ya Jinsia na Mahitaji Maalum katika Mradi wa HEET UDSM amesema, sera na miongozo hii imekuwa ikishughulikiwa na timu za wataalamu katika maeneo husika na kwamba kwa sasa iko katika hatua mbalimbali za kuidhinishwa na mamlaka husika.

Dkt. Mahai amesema miongozo ambayo inaandaliwa ni pamoja na mwongozo wa kushughulikia ukatili wa kijinsia na unyanyasaji wa kingono pamoja na mwongozo wa namna ya kushughulikia malalamiko. Ameendela kusema kwamba sera ya kupinga unyanyasaji wa kingono ya mwaka 2018 itafanyiwa mapitio.

Dkt. Lulu Mahai amefafanua zaidi kwamba mapitio ya sasa ya Sera ya Kupinga Unyanyasaji wa Kingono ya mwaka 2005 yamefanyika kwa lengo la kukishirikisha moja kwa moja Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kama mdau muhimu pamoja na watu wengine wote ambao kwa namna moja ama nyingine wanahusiana na Chuo.

“Lengo la Sera hii ni kujenga mazingira rafiki ya ufunzaji na ujifunzaji ambapo wanajumuiya wote na watu wengine watakaokutana nao watakuwa huru na salama kufanikisha mahitaji yao ya kitaaluma na mengine yanayohusiana na hayo. Dhamira hii inaakisiwa vyema katika maadili ya msingi ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kama yalivyoakisiwa katika hatiidhini ya Chuo”, amesema Dkt. Mahai.

Dkt. Mahai anasisitiza kwamba kupitia sera hizi na miongozo mingine inayohusiana nayo, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kitaendelea kubaki katika ubora wake ya kuwa mazingira salama yanayozingatia haki na usawa wa kijinsia ambapo wadau wa ndani na nje wanakutana huku wakijenga imani na heshima kwa kila mtu na kukifanya Chuo kuwa katika mazingira yanayozingatia utu na masuala ya kijinsia.

Ameeleza kwamba miongozo ya kushughulikia ukatili wa kijinsia na unyanyasaji wa kingono inalenga kuhakikisha kwamba kunakuwa na mazingira tulivu na yenye uhuru wa kufanya kazi na kujifunzia ambayo yanazingatia usawa wa kijinsia na kuondoa viashiria vyovyote vya unyanyasaji, udhalilishaji na ukatili wa kijinsia.

“Miongozo hii inabainisha mfumo thabiti wa namna ya kushughulikia udhalilishaji wa kijinsia na kingono katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Kupitia miongozo hiyo wanajumuiya watafahamu wajibu wao hivyo, watakuwa mabalozi na watu wanaowajibika katika matendo yao dhidi ya watu wengine”, amesema Dkt. Mahai.

Dkt. Jackline Mgumia, Mtaalamu wa Jamii katika Mradi wa HEET UDSM amesema kwamba Mwongozo wa kushughulikia malalamiko Chuo Kikuu cha Dar es Salaam umeweka kanuni na hatua ya namna ambavyo malalamiko yatashughulikiwa katika ngazi zote za kiutawala Kikuu cha Dar es Salaam.

“Mwongozo utakiwezesha Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kuwa mfano bora wa kushughulikia malalamiko kwa amani na utulivu. Ni muhimu kwa wanajumuiya ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na wadau wengine wasome mwongozo na kuutumia wakati wa kushughulikia malalamiko mara yanapojitokeza”, Amesema Dkt. Mgumia.

Dkt. Mgumia amesisitiza kwamba mwongozo huu utasaidia katika utendaji wa haki na usawa wakati ufunzaji na ujifunzaji, utendaji kazi katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kwa kuwahusisha wadau wa ndani na nje ya Chuo.





*Dkt. Lulu Mahai*
*Mratibu wa Masuala ya Jinsia na Mahitaji Maalum, HEET-UDSM*



*Dkt. Jackline Mgumia, Mtaalamu wa Jamii, HEET-UDSM*

Chuo Kikuu cha Dar es Salaam

## Mawasiliano

Naibu Mratibu: +255 765 939 958
Mhariri Mkuu: +255 755 172 570

heet@udsm.ac.tz Heet Udsm www.udsm.ac.tz